

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



S.L.P 30261

Kibaha,

Simu: (023) 2402658

Nukushi: (023) 2402657

Barua pepe: rbcpwani@pccb.go.tz

Wavuti: www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

PWANI – JULAI 01, 2020

TAPELI AFIKISHWA MAHAKAMANI KWA KUJIFANYA AFISA WA TAKUKURU

Leo Julai 1, 2020 TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA Mkoa wa Pwani itamfikisha JOSEPH NEHEMIA MWENDA katika Mahakama ya Wilaya Kibaha kwa kosa la kushawishi na kupokea rushwa ya zaidi ya shilingi 15,000,000/= Kinyume na Kifungu cha 15 (a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007.

Mtuhumiwa huyu amefanikiwa kupata fedha hizo kutoka kwa mwananchi mmoja kwa madai kuwa fedha hizo zimeombwa na Afisa wa TAKUKURU ili aweze kumsaidia mtuhumiwa huyo katika kesi yake. Uchunguzi dhidi ya mtuhumiwa unaendelea.

WITO:

Ninawaasa wananchi kutoa taarifa mara watakapopigiwa simu na mtu yeyote atakayejitambulisha kuwa ni Afisa wa TAKUKURU na kumdai fedha au akitaka waonane eneo ambalo sio ofisi ya TAKUKURU.

KUKATAA KWAKO RUSHWA KUNA THAMANI

Imetolewa na:

SUZANA RAYMOND,
MKUU WA TAKUKURU MKOA
PWANI